

*palizi*

**Ukataji wa maua**

- Kata maua kusaidia majani kurefuka na kupanuka na pia kuongezeka kwa mizizi
- Kata maua ili wanga uliotengenezwa utumike na majani na kuyapa uzito
- Maua hutumia wanga mwingi ili kutengeneza mbegu na kusababisha majani kuwa mepesi

**Ukataji wa kuchelewa**

- Pale ambapo rutuba imezidi tumbaku huwa na rangi ya kijani nzito, hivyo ukataji wa maua hucheleweshwa kidogo ili rangi ya kijani ipungue

**Ukataji wa kawaida**

- Penye rutuba ya kawaida na mvua nzuri mkulima anaweza kukata maua na kuacha majani kulingana na aina ya mbegu iliyopandwa
- Kwa ujumla inashauriwa ukataji wa maua katika hali ya kawaida ufanyike wakati asilimia 30 hadi 50 ya mimea yote imefungua maua

**Uwekaji wa dawa ya kuzuia vikonyo**

- Mara baada ya kukata vitumba vya maua weka mchanganyiko wa dawa ya yamaoteo na maji
- Hakikisha dawa haikumwagikii kwenye ngozi na pia kwenye jani
- Iwekwe sehemu ilipokatwa kitumba tu
- Mkulima anashauriwa kuvaa gloves kwa ajili ya kujikinga na dawa isimwagike kwenye mikono



*Mmea uliokwatwa kitumba cha maua*

| Aina ya dawa | Dozi | Jinsi ya kuweka | Kuzuia |
|---|---|---|---|
| Yamaotea super (Flumentralin+Butralin) | Lita moja kwa hekta | Changanya mililita 8 za yamaotea katika lita moja ya maji (mililita 80 za yamaotea katika lita 10 za maji) | Vikonyo |

Njia ya uwekaji

- Njia inayopendekezwa ni kutumia hand apllied cups
- Njia inayofuata ni squeegee bottle
- Njia ya tatu ni knapsack applicati


KWA MAWASILIANO :

TAASISI YA UTAFITI WA TUMBAKU TANZANIA (TORITA)

S.L.P 431,

TABORA.

Barua pepe : info@torita.or.tz

Tovuti:*www.torita.or..tz*


JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA

## TAASISI YA UTAFITI WA TUMBAKU TANZANIA (TORITA)



# *Njia sahihi za uzalishaji wa tumbaku ya mvuke shambani*

**Faida za kuaanda shamba mapema**

- Kutunza maji kwenye udongo
- Kuwezesha kuozesha masalia ya mimea vizuri
- Kupunguza idadi ya wadudu na magonjwa

**Vipimo sahihi vya mashimo na matuta**

- Umbali kati ya tuta na tuta uwe wa sentimita 120
- Umbali kati ya mche na mche uwe wa sentimita 50
- Chimba mashimo makubwa sehemu ambampo umeweka alama . Hii ifanyike kabla ya mvua kunyesha
- Mashimo haya yatasaidia kuhifadhi unyevu .



*Maandalizi ya mashimo kabla mvua haijanyesha.*

Sifa za miche ya kupandikizwa

- Iwe ilivyokomazwa, ambayo haikumwagiliwa maji kwa wiki mbili kabla haijang'olewa
- Iwe na ukubwa unaolingana
- Iwe iliyong'olewa siku moja

Kupandikiza kwa kutumia mvua

- Pandikiza kama kuna mvua za kutosha. Maji ya mvua yawe yameingia kwenye udongo sentimita 40-50
- Mashimo yawe yamepata maji ya kutosha ka-bla ya kupandikiza
- Pandikiza miche sentimita 15-20 katikati ya shimo lililochimbwa
- Kandamiza udongo mara baada ya kupandikiza
- Miche isiyo na afya nzuri hufa na kulifanya shamba kuwa na mapengo
- Miche yenye afya nzuri hustawi na kulifanya shamba lionekane vizuri



Hatua za mwanzo za upandaji Tumbaku

| Aina ya dawa | Kiwango kwa hekta | Jinsi ya kuweka | Wadu-du wanao zuiwa |
|---|---|---|---|
| Decis, kidonge cha gramu 2 | Vidonge 12 kwa hekta | Weka nusu kidonge kwenye lita 10 za maji. Kwa kutumia sprayer nyunyizia kwenye kila mmea mara baada ya kupandikiza | Sota (cutworms) |
| Confidor (70WP) | Pkiti 7 kwa hekta sawa na gramu 210 kwa hekta | Yeyusha gramu 10 za pakiti ya gramu 30 katika lita 10 za maji. Nyunyizia mililita 14 kwa kutumia sprayer kwenye kila mmea mara baada ya kupandikiza | Chawa wa ma-jani (Aphids) |

Kuziba mapengo

- Ziba mapengo ndani ya siku saba mara baada ya kupanda ili miche ikue kwa kimo kinacholingana.
- Tumia lita 3 za maji kwa kila shimo kama hakuna mvua ndani ya hizo siku saba.
- Ziba mapengo kabla ya kuweka mbolea.



*Shamba ambalo halijazibwa mapengo*



Shamba lilozibwa mapengo

Mbolea ya kwanza

- Mbolea inayotakiwa ni NPK katika uwiano wa 10:18:24
- Weka mbolea mapema mara baada ya kupandikiza
- Mbolea iwekwe kwenye mashimo mawili moja kila upande wa mche na kufukiwa kwa udongo siku 7 hadi 10 toka siku ya kupandikiza miche
- Mbolea isiyofunikwa hupotea hewani kwa kuyeyushwa na jua
- Umbali toka kwenye mche hadi kwenye shimo la mbolea ni sentimita 10 kila upande
- Shimo la mbolea liwe na urefu wa sentimita 5 hadi 7
- Weka mifuko 10 (kilo 500) za NPK 10:18:24 kwa hekta

Mbolea ya pili

- Weka mbolea ya CAN kiasi utakachoshauriwa na bwana shamba kabla ya wiki 3 kupita baada ya kupandikiza



*Jinsi ya kuweka mbolea shambani*

Aina za palizi

- Kwa kutumia jembe la mkono palizi inaweza kufanywa mara mbili au zaidi
- Dawa ya kuua magugu inaweza kutumika wakati au baada ya kupanda miche ya tumbaku
- Tifulia tumbaku na jenga upya matuta, legeza udongo karibu na mimea ya tumbaku kuwezesha mzunguko mzuri wa hewa na mmea kunyonya lishe ya kutosha katika kipindi cha wiki 4 hadi 6 baada ya kupanda
- Hii ndiyo njia ya kukuza shina haraka

Muda wa kukata maua

- Kukatia chini

Katika hali ya uhaba wa mvua tumbaku hudumaa. Kata vitumba vya maua ili virutubisho vielekezwe kwenye majani ili yawe mapana na mazito

Tumbaku hii huwa fupi hivyo husemwa imekatiwa chini

Tumbaku inaweza kudumaa pia kutokana na kuzidi mvua